



## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



#### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI MDOGO WA UDIWANI KATIKA KATA NNE ZA TANZANIA BARA

Dodoma, 10 Septemba, 2021

Tume imepokea barua kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa akiitaarifu juu ya kuwepo kwa nafasi wazi za Madiwani kwenye kata nne (4) za Tanzania Bara. Nafasi hizo zilitokana na kufariki kwa Madiwani wa Kata 3 na mmoja kujiuzulu.

Kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 13 (2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume imeandaa Uchaguzi Mdogo ili kujaza nafasi za Udiwani kwenye Kata nne (4) za Tanzania Bara.

Kata hizo nne (4) za Tanzania Bara ni:

Na.	MKOA	HALMASHAURI	JIMBO	KATA
1.	Dar es Salaam	Jiji la Dar es Salaam	Ukonga	Buyuni
2.	Manyara	Wilaya ya Kiteto	Kiteto	Dongo
3.	Singida	Wilaya ya Ikungi	Singida Mashariki	Lighwa
4.	Shinyanga	Manispaa ya Shinyanga	Shinyanga Mjini	Ndembezi

Uchaguzi huu Mdogo wa Udiwani katika Kata nne (4) utafanyika sambamba na Uchaguzi Mdogo wa Ubunge wa Majimbo mawili (2) ya Konde, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba – Zanzibar na Ushetu, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu Mkoa wa Shinyanga Tanzania Bara pamoja na Kata sita (6) za Tanzania Bara ambazo ni Lyowa – Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Mkoani Rukwa, Kileo - Halmashauri

ya Wilaya ya Mwanga, Mkoani Kilimanjaro, Vumilia - Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, Mkoani Tabora, Neruma - Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Mkoani Mara, Luduga - Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Mkoani Njombe, na Kagera-Nkanda - Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoani Kigoma.

Ratiba ya Uchaguzi Mdogo wa Kata nne (4) Tanzania Bara itaenda sambamba na Ratiba ya Uchaguzi Mdogo wa wa Majimbo mawili (2) ya Konde, Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba – Zanzibar na Ushetu, Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu Mkoa wa Shinyanga Tanzania Bara na Kata sita (6) za Tanzania Bara ambayo ni kama ifuatavyo:-

Na.	TUKI	TAREHE
1.	Wagombea kuchukua fomu za uteuzi	13 - 19 Septemba, 2021
2.	Uteuzi wa wagombea	19 Septemba, 2021
3.	Kampeni za Uchaguzi	20 Septemba - 08 Oktoba 2021
4.	Siku ya kupiga kura	09 Oktoba 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea kuvikumbusha vyama vya siasa na wadau wote wa uchaguzi kuzingatia sheria, kanuni, maadili ya uchaguzi, taratibu, miongozo na maelekezo yatayotolewa na Tume katika kipindi cha uchaguzi huo mdogo.

  
Dkt. Wilson Mahera Charles

**Mkurugenzi wa Uchaguzi**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**